**Tume ya Afrika kukataa Ombi la kihadhi la mashirika ya haki za kibinadamu inatishia uwezo wake wa kutekeleza jukumu la kukuza na kulinda haki za kibinadamu**

Sisi, kama mashirika wasahihi, tunasikitika na uamuzi wa Tume ya Afrika Ya Haki za Binadamu na Watu wa kukataa ombi la kihadhi la mashirika matatu yakiwa Alternatives Cote d'Ivoire, Human Rights First Rwanda na Synergia – Initiatives for Human Rights. Katika tangazo rasmi baada ya kikao cha 73 kilichofanyika Banjul-Gambia, kuanzia tarehe 20 Oktoba hadi 9 Novemba, 2022, tume hii ilitangaza kupuuzilia mbali ombi la mashirika haya matatu kwa msingi kwamba mwelekeo wa kijinsia hautambuliki waziwazi kama haki au uhuru chini ya Mkataba wa Afrika na kwamba ni kinyume na maadili ya Kiafrika.

Tunaamini kwamba uamuzi huo unaendeleza ubaguzi na ukosefu wa mshikamano katika jamii. Uamuzi wenyewe una athari hasi dhidi ya juhudi za kukomesha ukiukaji wa haki za kibinadamu, watu na jamii kwa msingi halisi au unaofikiriwa kuhusu mwelekeo au utambulisho wao wa kijinsia ama kueleza uana wao. Uamuzi huu haudhibitishi chuki dhidi ya watu wa jinsia moja au wa jinsia tofauti barani Afrika pekee, bali pia unahatarisha watetezi wa haki wanaotetea wasagaji, mashoga, waliobadili jinsia zao na wenye jinsia mbili tofauti (LGBTI). Watetezi hawa sasa wako katika hatari ya kudhulumiwa na kubaguliwa na watendaji wa serikali na wasio wa serikali.

Uamuzi huo wa Tume ya Afrika umejitenga na hatua za kuwalinda wasagaji, mashoga, waliobadili jinsia zao na wenye jinsia mbili tofauti ikiwemo mageuzi ya sheria na maamuzi ya kiutendaji na ya mahakama yanayohalalisha mahusiano ya jinsia sawa miongoni mwa watu wazima. Mfumo huu umekubaliwa na mataifa mengi ya Kiafrika kama: Angola, Botswana, Cape Verde, Cote d' Ivoire, Gabon, Malawi, Mozambique, Seychelles na Afrika Kusini.

Mashirika ya Kiafrika na kimataifa yana jukumu la kuhakikisha mashirika yasiyo ya kiserikali na na mashirika ya kiraia wameshirikishwa na kwamba haki zao za kushiriki zimeheshimiwa. Ufanisi katika utendaji wa majukumu ya mashirika ya Kiafrika na kimataifa unategemea kushirikishwa kwa mashirika ya kiraia. Kushiriki kwa mashirika yasiyo ya kiserikali hauwezi kutenganishwa na haki ya kushiriki katika uendeshaji wa masuala ya umma na vilevile, uhuru wa kujieleza, mikutano ya amani na ushirika. Hizi ni haki za binadamu zinazolindwa na mikataba kadhaa ikiwemo Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (African Charter on Human and Peoples' Rights) na Agano la Kimataifa la Haki za Kiraia na za Kisiasa (International Covenant for Civil and Political Rights). Haki hizi lazima zifaidi kila mtu bila ubaguzi wowote, ikiwemo kwa msingi wa mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia au kujieleza kwa jinsia na sifa za kimaumbile za kijinsia.

Kwa kukataa ombi la mashirika haya matatu, Tume ya Afrika imetofautiana na kuenda kinyume na sheria za utendaji wake wa kawaida. Tume hii imeonyesha kwamba 'hadhi nyingine' kama inavyorejelewa na kifungu cha 2 cha Mkataba wa Kiafrika, haijaishia kwa msingi uliopendekezwa kwenye mkataba huo, ila imeendelezwa kwa masuala mengine likiwemo 'mwelekeo wa kijinsia'. Kwa kweli katika uamuzi wa Tume ya Afrika katika kesi ya *Zimbabwe Human Rights NGO Forum v Zimbabwe* (Tangazo Nambari 245/2002), Tume ya Afrika iliamua kwamba lengo la kifungu hicho cha 2 ni kuhakikisha usawa kwa wote bila kujali uraia, jinsia, kabila, maoni ya kisiasa, dini, imani, ulemavu, umri au mwelekeo wa kijinsia.

Aidha, katika *azimio la 275 ya ulinzi dhidi ya unyanyasaji na ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya watu kwa msingi wa hisia au jinsia (ACHPR/Res.275(LV)2014),* Tume hii ilikumbuka kuwa Mkataba wa Kiafrika imepiga marufuku ubaguzi dhidi ya yeyote kwa msingi wa tofauti za aina yoyote kama vile: rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, mielekeo yoyote au ya kisiasa, asili ya kijamii au kitaifa, bahati, uzawa au hadhi yoyote. Tume hii pia ikumbuke kwamba kifungu cha 3 cha mkataba kinampa kila mtu ulinzi sawa kisheria.

Tume ya Afrika bila shaka imedhibitisha kwamba dhamana chini ya kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba wa Kiafrika (ya uadilifu wa mtu na inayopiga marufuku kutesa, kunyanyasa na kudunisha mtu) lazima ifaidi kila mmoja bila kujali mwelekeo au utambulisho wake wa kijinsia. Tume hii inatambua kwamba LGBTI pia wana haki chini ya mkataba huu na wanapaswa kufaidi haki hizi, ikiwemo haki na uhuru wa kutangamana bila ubaguzi wowote. Tume yenyewe imeonyesha kwamba uhuru wa kutangamana lazima ueleweke kwa namna inayolingana na sheria za haki za kikanda na kimataifa. Hivi sasa ni kanuni imara kwamba ubaguzi kwa msingi wa mwelekeo wa kijinsia umepigwa marufuku; tume hii inapaswa kushikilia kanuni hii katika maamuzi yake.

Kwa kukataa maombi ya kihadhi ya hayo mashirika matatu, Tume ya Kiafrika inakanusha kwamba watu wanaolinda haki za wasagaji, mashoga, waliobadili jinsia zao na wenye jinsia mbili tofauti (LGBTI) wanaweza kuwa watetezi wa haki za kibinadamu, kinyume na Azimio la 376/2017 ya Hali ya Watetezi wa Haki za Kibinadamu Barani Afrika (*Resolution 376/2017 on the Situation of Human*

*Rights Defenders in Africa)* ambayo Tume yenyewe ilitoa wito wa kupitishwa kwa hatua maalum za kisheria za kutambua hadhi ya watetezi wa haki za kibinadamu na kulinda haki zao, za wenzao, jamaa zao wakiwemo watetezi wa haki za wanawake na wanaoshughulikia masuala kama mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia.

Tume hii kurejelea maadili ya Kiafrika, si unukuzi mbaya tu wa Mkataba wa Afrika, bali pia ni kujitenga na mkataba wenyewe. Wakati kifungu cha 29(7) kinasema kila mtu ana jukumu la kuhifadhi na kuimarisha maadili mema ya kitamaduni za Kiafrika na kwa mahusiano yake na raia wengine, na kwa moyo wa uvumilivu, mazungumzo na mashauriano na kuchangia kukuza maadili ya kijamii, ni vigumu kuamini kukana kufurahia haki na uhuru zinazotambulika na kuhakikishwa na Mkataba wa Kiafrika kwa mwenye-haki yeyote bila ubaguzi, wakiwemo watu wa LGBTI, ni 'maadili chanya ya Kiafrika' inayolindwa na mkataba.

Katika tangazo lake rasmi, ilionekana Tume hii ilikataa kanuni msingi ya ulimwengu mzima ya haki za kibinadamu, iliyowekwa na Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu kama kanuni msingi ya vifaa na utaratibu wa haki zote. Kwa jinsi hii, utangulizi wa Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu unatambua heshima ya kiasili na haki sawa za kiugeni kwa familia za kibinadamu. Uamuzi wa Tume hii, kwa hivyo, ni kinyume na mwelekeo wa kifungu cha 60 cha Mkataba wa Kiafrika kinachosema kuwa, Tume itapata msukumo kutoka kwa sheria za kimataifa za haki za watu, haswa masharti kutoka kwa asasi mbalimbali za haki za kibinadamu, Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu na asasi nyingine iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa na Mataifa ya Kiafrika katika mrengo wa haki za watu na za kibinadamu.

Rajua, maono na jukumu la mashirika haya matatu haijumuishi tu haki za wasagaji, mashoga, waliobadili jinsia zao na wenye jinsia mbili tofauti (LGBTI) na watetezi wa haki hizi. Kwa kukataa ombi lao, Tume hii inapitisha ujumbe wa kutisha kwa watetezi wa haki barani, kwamba ulinzi wa haki za wasagaji, mashoga, waliobadili jinsia zao na wenye jinsia mbili tofauti (LGBTI) na watetezi wa haki hizi utazuia nafasi zao za kushiriki katika masuala ya umma na mfumo wa Kiafrika. Mbinu kama hiyo ni tofauti kabisa na azimio la 275 linalohimiza mataifa kuhakikisha watetezi wa haki wana mazingira yanayowafaa; huru kutokana na unyanyapaa, kisasi, mashtaka ya jinai. Uamuzi wa Tume hii unalemaza azimio la 275 kwa kuwa inadhalilisha yeyote anayefanya kazi kuifanya iwe kweli.

Utaratibu wa uamuzi wa Tume pia ni tofauti na viwango vyake vya utendaji vya kuzingatia ombi la mashirika haya katika kikao cha umma. Muhimu zaidi, Tume ilichapisha uamuzi wao wa kukataa maombi ya mashirika haya matatu katika tangazo rasmi baada ya kikao chake cha 73 bila kuwajulisha mashirika haya. *Azimio 361 la kutoa na kudumisha hadhi (Observer Status) kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na inayohusika na haki za kibinadamu barani Afrika,* lahitaji wazi Tume ya Kiafrika kujulisha washirika walio omba hadhi hizi kuhusu uamuzi wao bila kuchelewa.

Tuna wasiwasi kuwa uamuzi wa Tume hii unaweza kuwa umechochewa na uamuzi nambari 1015 wa Halmashauri Kuu asasi ya kisiasa kwenye Muungano wa Kiafrika ambayo hapo awali ilishinikiza Tume ya Kiafrika kutoa hadhi iliyopewa Coalition of African Lesbians. Kwa hiyo, uamuzi huu haupendekezi tu utabiri wa Tume hii wa kufurahisha wanachama wachache wakandamizi, bali pia unaashiria mwelekeo hatari usioweza kukombolewa na kuachia uhuru wake wa kutekeleza jukumu lililowekwa na kifungu cha 45 cha Mkataba wa Afrika. Uamuzi huu unatia shaka uadilifu, kutokuwa

na upendeleo na ujuzi kuhusu haki za kibinadamu ya wanachama wa Tume ya Afrika inavyohitajika na kifungu cha 31 cha mkataba.

Kwa misingi hii, mashirika ambayo yametia sahihi yanahimiza Tume ya Afrika:

- kurejesha mara moja uamuzi wa kukataa ombi la hadhi ya mashirika haya matatu na kutekeleza wajibu wake wa kulinda na kuendeleza haki kwa kila mtu kama inavyoelekezwa na kifungu cha 45 cha Mkataba wa Afrika;
- kuhakikisha imeheshimu, imelinda na kutimiza haki za kibinadamu kulingana na viwango vya sheria za kimataifa na kikanda bila kuingiliwa na maoni ya kisiasa na kushikilia uhuru wake katika kufanya maamuzi;
- kudhibitisha tena azimio la 275/2014 katika maamuzi yake yote na kutambua hatari ya vurugu na aina yoyote ya ubaguzi dhidi ya watu kwa msingi halisi au unaofikiriwa kuhusu mwelekeo na utambulisho wao wa kijinsia;
- kujitolea kuwalinda watetezi wa haki za kibinadamu bila ubaguzi wowote;
- kuepuka fasiri zozote za Mkataba wa Afrika zilizo na vikwazo na zinazoweza kuathiri wajibu wao wa kulinda na kukuza haki za kibinadamu kwa wote.

**Wafadhili wakuu wa Kauli**

*African Union Watch*
*Alternative Côte d'Ivoire*
*Amnesty International*
*Article 19*
*Centre for Human Rights – University of Pretoria*
*Civicus*
*Commission indépendante des droits de l'homme en Afrique du Nord*
*DefendDefenders*
*Equality Now*
*Human Rights First Rwanda*
*Human Rights Watch*
*Institute for Human Rights and Development in Africa*
*International Federation for Human Rights*
*International Service for Human Rights*
*Le Mouvement pour les Libertés Individuelles*
*PanAfrica ILGA*
*Robert F. Kennedy Human Rights*
*Synergía – Initiatives for Human Rights*
*The Initiative for Strategic Litigation in Africa*
*International Federation for Human Rights*

Kuunga mkono kauli hii, bonyeza hapa.